

26 June 63 MWAFRIKA

Kawawa asuta Amerika na Uingereza

ACHENI URAFIKI NA ADUI ZETU

Ripota wetu, Dar es Salaam; Jumano.

A KISEMA KWA UKALI, MAKAMU WA RAIS YA JAMHURI YA TANGANYIKA, BW. RASHIDI KAWAWA LEO ALIZISHAMBULIA VIKALI NCHI ZA UINGEREZA NA AMERIKA KWA KUENDELEA KUFANYA BIASHARA NA MKABURU PAMOJA NA MRENO.

Bw. Kawawa alikuwa akifungua mkutano wa nchi tisa za Afrika huru zenye madhumuni ya kupanga mpango wa kumaliza ukoloni katika Afrika, unaofanywa mjini Dar es Salaam.

Makamu huyo alisema kwamba Uingereza na Amerika 'ndio marafiki wakubwa wa maadui zetu.'

Urafiki na adui:

Akitaja hesabu ya biashara kati ya nchi hizo na Afrika ya Kusini, alidokeza kuwa hesabu aliyotaja ilionyesha kwamba ingawa UNO imepitisha maazimio na pia ulimwengu umeilani nchi hiyo, lakini nchi hizo mbili zinafanya urafiki na maadui zetu.

Bw. Kawawa alionya kwamba katika mapambano ya kuondoa ukoloni yanayokuja, hatutakuwa na msalie mtume. 'Nchi hizo aidha zitakuwa nasi, au zitakuwa kinyume na sisi, na wala hakutakuwa na mtu kujidai hayuko huku wala kule,' alitamka.

Alisema pia kwamba itakuwa sio haki kusema kuwa hakuna biashara ndogo inayotoka nchi nyingine na Afrika ya Kusini, lakini Tanganyika ingetaka hata hiyo biashara ndogo nayo iachwe.

Akijibu hotuba ya Bwana Kawawa, Waziri wa Mambo ya Kigeni, katika nchi ya Nigeria, Bw. Jaja Wachuku, alisema, 'wakati wowote, basi nchi huru za Afrika zinakuwa kama ndege anaeruka kwa bawa moja.'

Waziri huyo alisisitiza kwamba nchi za Afrika ziko tayari kujitoa kwa njia zote, ili kutafuta dawa ya kuondoa ukoma huu katika Afrika.

Akaongeza, 'tumekuwa hapa kufanya kazi nzuri, na hiyo ni kutoa mipango ya mapendekezo yaliyofanywa mjini Addis Ababa.'